*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## Kikao cha Kwanza – Tarehe 31 Machi, 2020

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

## WIMBO WA TAIFA

*(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)*

## WIMBO WA JUMUIYA YA AFRIKA MASHARIKI

*(Hapa Wimbo wa Jumuiya ya Afrika Mashariki Uliimbwa)*

## D U A

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, *Asalaam Aleykum;* Bwana Yesu Asifiwe; tumsifu Yesu Kristu.

Naomba niwakaribishe tena Dodoma baada ya likizo ambayo tumekuwa nayo na baada ya kazi kubwa ambayo mmeifanya kupitia Kamati mbalimbali za Bunge; kutembelea mikoani na kurudi hapa Dodoma. Karibuni tena siku ambayo tunaanza rasmi Mkutano wetu wa Kumi na Tisa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mkutano wa Bajeti, ambao ndiyo Mkutano wetu wa mwisho kwa Bunge hili la Kumi na Moja.

Safari tunayoianza leo ni safari ndefu ambayo tunatarajia inaweza ikaenda hadi tarehe 30, Juni. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aibariki nia yetu hiyo ili kila tulichokipanga kiweze kutekelezeka.

Leo hatuko na Mheshimiwa Waziri Mkuu asubuhi hii, ana udhuru, yupo Dar es Salaam. Kama mnavyojua yeye ndio Mratibu Mkuu wa masuala yote yanayoendana na janga hili la ugonjwa huu wa Corona ulioingia hapa nchini. Kwa hiyo, kuna kazi maalum, lakini ametutumia salamu na niwahakikishie kesho tutakuwa naye *inshallah.*

Pia niwape salamu za Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, anatutakia kila la heri katika kazi zetu tunazozianza leo na yupo nasi hatua kwa hatua. Kama mnavyojua, siku ya mwisho ya Bunge hili atakuja kuzungumza nasi; na msishangae siku yoyote katikati hapa siku moja tukawa naye katika mazingira haya. *(Makofi)*

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Naomba nitoe taarifa chini ya Kanuni ya 33(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kwamba katika Mkutano uliopita wa Kumi na Nane wa Bunge, Bunge lilipitisha Miswada miwili ya Sheria ya Serikali ifuatayo:-

Kwanza Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 8 wa Mwaka 2019 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 8) Bill 2019]* na wa pili ni Muswada wa Sheria ya Usuluhishi wa Mwaka 2020 *(The Arbitration Bill, 2020).*

Kwa taarifa hii, napenda kuliarifu Bunge hili Tukufu kwamba tayari Miswada hiyo miwili imepata kibali cha Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa kibali hicho cha Mheshimiwa Rais sasa ni Sheria za Nchi zinazoitwa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali, Sheria Na. 1 ya Mwaka 2020 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act No. 1 of 2020)* na ya pili ni Sheria ya

Usuluhishi (Na. 2) ya Mwaka 2020 *(The Arbitration Act (No. 2) of 2020).*

Baada ya taarifa hiyo ya Spika, nielekeze tu kwamba majuzi hapa, Waheshimiwa Wabunge natumaini mlifuatilia; baadhi yetu tulialikwa pale Chamwino, Ikulu ambapo Mheshimiwa Rais alikuwa akipokea taarifa mbili muhimu: Moja ya TAKUKURU na nyingine ya *Controller and Auditor General.*

Mheshimiwa Rais alielekeza pale kwamba ni vyema taarifa zile zikashughulikiwa katika kipindi hiki. Kama mnavyojua mwaka huu una kalenda ya uchaguzi, kwa hiyo, wakati wa kusema Kamati zetu zitashughulikia masuala yanayoendana na hoja za ukaguzi unaweza usiwepo baadaye. Kwa hiyo, tutajitahidi, tujibane ili ndani ya Bunge hili tuweze kushughulikia hoja zilizokuwa *raised* ndani ya Ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali *(CAG)* katika kipindi hiki hiki.

Kwa hiyo, tunawaomba wenzetu Serikalini waandae majibu haraka iwezekanavyo, lakini majibu yote hayo yapelekwe kwa *CAG* kwanza kwa ajili ya *verification* na kadhalika, ili baada ya muda siyo mrefu tupange ratiba ya ndani ili kuhakikisha kwamba Kamati zetu zile za ufuatiliaji *(Public Accounts na Local Authorities Accounts Committees)* zinafanya kazi yake na ikiwezekana mwisho wa Bunge hili, moja ya shughuli zetu iwe ni kukamilisha shughuli nzima ya Ripoti ya *CAG.*

Uendeshaji wetu wa shughuli za Bunge utakuwa na mabadiliko makubwa; na mabadiliko mengi tayari tumeshawatumia Waheshimiwa Wabunge kupitia *tablets* zetu, kwa hiyo, mnayo. Tutakuwa tukiongea na wananchi pia wakati kwa wakati.

Nipitie tu machache kwa juu juu sana kwa sababu tayari mnayo. Mabadiliko haya yanatokana na tatizo hili la kukabiliana na Ugonjwa wa Corona katika mazingira ambayo lazima pia Bunge litekeleze wajibu wake wa kuwatumikia wananchi na wajibu wake wa Kikatiba.

Jambo la kwanza ambalo tunawasisitiza Waheshimiwa Wabunge na wadau wote wanaokuja hapa Bungeni ni suala zima la kuwa na umbali kati ya mtu na mtu kadri iwezekanavyo. Kwa hiyo, hatutarajii humu ndani kuona watu wawili watatu wamebanana na kadhalika. Tutakuwa na utaratibu ambao utawezesha kila Mbunge kupata nafasi ya kushiriki shughuli za humu ndani na maeneo mengine ambayo tumeyatenga.

Kama mnavyofahamu tayari tumeimarisha kumbi mbalimbali ili uendeshaji wetu uweze kuwa mzuri. Hata Dawati la Spika limebadilika sasa, limekuwa na teknolojia kadhaa, limesheheni mambo hapa. Ninaweza kuona ukumbi huu vizuri zaidi bila kulazimika kutazama huko. Pia naweza nikaona kumbi nyingine zote ambazo tumeziandaa kwa ajili ya uendeshaji wa mambo hapa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kitu muhimu ni hicho wanaita kwa Kizungu *social distance;* inasisitizwa sana katika maisha yetu, kote tunapokuwa na hata tunapokuwa katika mazingira ya Bunge, nami nasisitizia hilo hilo. Tumeshauriwa sana na wataalam tufuate taratibu za kunawa, kutumia *sanitizers* na nyingine zote tunazoshauriwa na Wizara ya Afya na tunazoshauriwa na Serikali yetu kwa ujumla na wataalam wa afya. Tuzingatie sana Waheshimiwa Wabunge na tuwahimize wananchi wetu kuzingatia kadri wawezavyo.

*Social Distance* siyo kitu kipya katika maisha ya mwanadamu. Hata mnyama ana *social distance.* Wewe kukutana na mkwe wako huwezi ukaegemeana naye hivi, kuna *social distance.* Eeh, ndiyo! Mama mzazi akikaa hapa na wewe mtu mzima huwezi kwenda tu kukaa pale, kuna *social distance. Social distance* hii huwa haiko *fixed,* inategemea mtu na mtu; huwa ina-*vary;* kuna mtu inapanuka, kuna mtu ina-*shrink,* lakini ndiyo maisha yetu. Hata wanyama wa porini wana *social distance.* Mpitie kuku jike wa kawaida, utapita tu, yuko hapa karibu; mpitie akiwa na vifaranga hapo katika *distance* ile ile, utaona shughuli yake; ni kwa sababu umeingilia *social distance* ambayo ni *not allowable.*

Hata nyoka akiwa na umbali ule kule, wewe unapita hapa, hana shida. Hata simba ana umbali fulani utapita, hana shida; lakini wewe msogelee ndani ya *social distance* fulani ambayo haikubaliki kwake, utamtambua kwamba yeye ni simba, au tembo au mnyama fulani.

Hata binadamu wako hivyo hivyo. Hata wawe ndani ya daladala wamesimama mle wamebanana, lakini kila mtu ana ka-*distance* kake. Wewe jaribu tu kugusa, utasikia wewe namna gani bwana! Kwa sababu tumeumbwa hivyo na Mungu. Sisi viumbe wote tuna *social distance* na huwa ina-*vary* kutegemeana na *situation* na hali halisi na mazingira uliyopo na aina ya mtu unaye-*interact* naye na kadhalika.

Sasa Corona nayo inahitaji *social distance* fulani. Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba siyo kitu kipya, ni ku-*adapt* tu na kukubali kwamba sasa ni ku-*observe social distance* angalau ya mita moja *or so* na mengine tuweze kuyafanya. Maana yake wengine wanaona kama hii ni taabu sana, lakini ni jambo ambalo linawezekana kabisa. Kwa hiyo, humu Bungeni tunaomba kwa kadri iwezekanavyo tu-*observe social distance.*

Kwa hiyo, idadi ya siku za Mkutano wetu zitabakia vilevile kama mikutano mingine ya bajeti ambapo itakuwa kuanzia leo, tarehe 31 mpaka tarehe 30, mwezi Juni, 2020. Muda wa vikao vya Bunge tutaubadilisha ambapo sasa kuanzia kesho tutakutana kuanzia saa 8.00 mchana hadi saa 12.00 jioni ili wale wanao-*observe* Kwaresma waweze kufanya hivyo na baada ya muda siyo mrefu, Kwaresma inapoisha wenzetu Waislamu nao wanaanza kufunga Mwezi wa Ramadhani; na wenyewe tunashauriwa tumalize saa 12.00. Kwa hiyo, tutaanza saa 8.00 na kumaliza saa 12.00. Tutajaribu sana hizi *four hours* kwa kila siku ya kazi tuweze kutekeleza kazi zetu.

Kila siku asubuhi randama na makabrasha mengine yote ambayo yanahitajika kwa Wizara hiyo yatatumwa *online* kuja kwenye *tablets* zenu. Pia namshauri Katibu wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge ambao wana *e-mail addresses*

tutume kwenye *e-mails* zao ili popote pale walipo Tanzania waweze kupata hizo randama na kama wana ushauri wowote wanaotaka kuutoa kwa maandishi waweze kuandika kuja kwenye Ofisi ya Bunge kwa Katibu na Katibu ata-*forward* moja kwa moja kwa Wizara au Waziri anayehusika na Wizara majibu yao pia watapitisha kama kuna haja ya kufanya hivyo kufuatana na maelekezo tutakayopeana kupitia Ofisi ya Katibu; pia na Ofisi ya Katibu nayo itampelekea ama Mbunge *specifically* ama sisi wote kutegemea na jambo lenyewe litakavyokuwa. Kwa hiyo, kwa upande huo tutakuwa vizuri kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, muda wa asubuhi mpaka saa 7.00 mchana matarajio yetu ni kwamba, kwa sababu mtakuwa na hizi taarifa zote, mtazitumia kupitia kusoma, kuelewa mapendekezo ya Serikali ni nini kuhusiana na bajeti inayohusika na kutengeneza maoni yenu. Kwa wale wanaochangia, basi waweze kujiandaa vizuri popote pale watakapokuwa; iwe kwenye maktaba yetu au maeneo mengine ambayo tumetenga, kuweza kujiandaa vizuri.

Mabunge mengi ya kwenye Jumuiya ya Madola yanatumia utaratibu huu wa kuanza Bunge mchana ili kutoa nafasi kwa Kamati za Bunge kuweza kukutana asubuhi, labda kuna jambo kuhusu Wizara hiyo, lakini pia inawapa nafasi Waheshimiwa Mawaziri kuwahi maofisini kwao na kuona madawati yao yakoje, ku-*organise* dawati lake ili anapokuja saa 8.00 hapa angalau kidogo anakuwa na amani kuliko ile ya asubuhi asubuhi anakuja huku, dawati kule nalo linamhitajia, inakuwa kidogo ni vitu vinaingiliana.

Tunajaribu, tumelazimishwa na ugonjwa huu kufikia hapa, lakini inatupa nafasi vilevile ku-*test* mitambo fulani fulani kwa Bunge la Kumi na Mbili kuona kama kutakuwa na haja ya taratibu zetu kuziangalia upya kuhusiana na namna ya uendeshaji. Kwa hiyo, naomba kwa hili tuvumiliane tu, twende twende kidogo, lakini tutakuwa tunapokea maoni yenu na kubadili taratibu zetu kadiri mnavyotushauri Waheshimiwa Wabunge, Waheshimiwa Mawaziri na wananchi kwa ujumla wake.

Uingiaji wa humu ndani utaandaliwa na Ofisi ya Katibu kwa kuzingatia na kushirikiana na ma-*Chief Whip* wa kila upande. Tutakuwa tunajua ni akina nani na watakuwa na taarifa. Kama mtu hayupo, basi ma-*Chief Whip* watatufanyia *substitution* ya nani aingie nani asiingie na kadhalika. Pia na Meza ya Spika nayo inaweza ikaruhusu mtu kama kuna sababu maalum na kadhalika ya kuweza kuingia zaidi ya ile orodha ya Wanadhimu.

Matarajio yetu ni kwamba, kwa wakati mmoja hatutazidi Wabunge 150 kwa kukaa kwa nafasi. Maana tukiwa tumejaa kabisa humu ndani ni 393, nadhani tusipozidi 150 bado ile *social distance* tutakuwa tumei-*observe.* Kwa wale Wabunge ambao hawatakuwa nasi hapa wakati Bunge likiendelea, tumeandaa hizo kumbi mbalimbali ambazo tumeweka *facilities* zikiwemo *television* ili kuweza kufuatilia kwa ukaribu na kama wana jambo lolote, wanaandika.

Tunawashauri Waheshimiwa Mawaziri safari hii kuja na timu za wataalamu wa *IT* wa Wizara zao. Wawapange huko ili ile *interaction* iweze kwenda vizuri *back and forth* kwa pande zote.

Pia kantini kwetu kutakuwa na matangazo ya moja kwa moja pamoja na hizo kumbi nyingine. Nashauri sana, *canteen* pawepo pia na utaratibu wa *take away* ambapo Mbunge anaweza akachukua anachokihitaji na akaondoka nacho au akaendelea kupata kitu chake huko kwenye ukumbi mwingine ambapo anaendelea kufuatilia bila kumwaga mwaga na kadhalika. Itasaidia zaidi katika kupunguza msongamano pia.

Utaratibu kuhusu maswali. Maswali yote kwa Mkutano huu yatajibiwa kwa utaratibu wa maandishi ambao pia maswali na majibu ya siku hiyo yatarushwa kwa Waheshimiwa Wabunge asubuhi ya siku hiyo. Kuanzia wakati huo yule tu mwenye swali lake kama ana swali la nyongeza anaweza kuliandika katika mfumo wetu wa kibunge likamfikia Katibu na Katibu atapeleka kwenye Wizara inayohusika na Wizara

wanapaswa kujibu maswali ya nyongeza kabla ya saa 7.00 ya siku hiyo hiyo kwa sababu ni maswali ya nyongeza ambapo huko nyuma tulikuwa tunajibu tu papo kwa papo.

Mbunge utakuwa umeyapata majibu *by* saa 7.00 ya siku hiyo, lakini kwa Mbunge mwingine yeyote, ile fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza hatutakuwanayo kwa sababu hatuna fursa hiyo. Tunampa tu yule mwenye swali lake la msingi, halafu tutaona na kushauriana huko mbele namna gani zaidi ya kuboresha utaratibu huo. Hatutakuwa na maswali kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ya papo kwa hapo katika kipindi hiki cha Mkutano wa Kumi na Tisa.

Utaratibu wa uendeshaji tutauelezea kadiri tutakavyokuwa tukiendelea na tutawatumia kwenye *tablets* zenu, pia Waheshimiwa Mawaziri waweze kujua utaratibu utakavyokuwa. Mawaziri wote wataongelea kwenye meza zao pale pale walipo, kwenye *microphone* zao na Wabunge pia mtaongelea kwenye *microphone* zenu. Hakuna yeyote atakayekuja kwenye hizi za pamoja ili kupunguza kidogo hali ile ambayo tunashauriwa.

Utaratibu wa kupiga kura tumeeleza pia kwamba ukifika wakati wa kupiga kura, wale ambao mtakuwa ndani ya ukumbi na wale ambao watakuwa nje ya ukumbi mtapiga kura ya Ndiyo na Siyo kwa kubonyeza kitufe ambacho kimo ndani ya *tablets* zenu. Mkibonyeza kile kitufe, basi mimi nitakuwa naona hapa kadiri mnavyobonyeza, zitakuwa zinanionesha moja kwa moja ni watu wangapi ambao wameikubali bajeti ya Wizara hiyo, watu wangapi ambao wamepiga kura za hapana na ikihitajika hata na majina yao nitakuwanayo. Kwa hiyo, kwa wale waliokuwa wanasema nyuma kule kwamba, kura za ndio, hapana, hazina uhakika na nini, safari hii tunaenda na mfumo ambao ni wa uhakika, wa moja kwa moja. Basi baada ya hapo nitatangaza matokeo ya kura hizo na bajeti hiyo itakuwa imepita.

Kwa kweli, kutakuwa na mabadiliko mbalimbali ambayo kadiri tutakavyokuwa tunaenda kuanzia kesho tutaona na tutaelezana, lakini hatutabadilika sana kutokana

na uendeshaji wetu. Tutajitahidi sana uendeshaji wetu uwe *almost* ni ule ule unaozingatia mambo mbalimbali.

Waandishi wa habari pia watakuwa wanaingia kwa zamu, wachache wachache kwa kadiri itakavyopangwa na Ofisi ya Katibu wa Bunge. Hatutakuwa na wageni kwenye *galleries* zetu, isipokuwa wachache sana labda kwenye *gallery* ya Spika watakaotutembelea kwa sababu maalum, lakini makundi ya wageni tunaya--*discourage* kwa sasa.

Tunataka punguzo la watu humu ndani kwa kila sekta *including* watumishi wetu wa Bunge, hata *page boys* na *page girls* watakuwa ni nusu ya wale ambao huwa wanakuwemo humu kwa kawaida. Tutawaomba hata madereva wa magari yenu, tutamwomba Katibu atenge eneo kule nyuma ambalo watumishi huwa wana-*park* magari na maeneo mengine wawe wakishawashusha Mawaziri na watu wengine wawe wanaenda ku-*park* kule nje ili nao wakae huko. Mheshimiwa Waziri ukitoka, unampigia simu, anaingia anakuchukua unaondoka, *except* Waziri Mkuu na wachache wengine. Yote hii tunatawanya watu na kufanya tusiwe na *concentration* kubwa humu ndani.

Baada ya maelezo hayo ya Spika, nitatoa nafasi mbili, tatu, nne kama kuna maswali ya ufafanuzi ili tuweze kufafanua hapa na baada ya hapo tutaahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa 8.00 mchana.

Kama kuna jambo la kukumbushana sote; nimepata wawili. Basi waishie hao hao. Kule nyuma kuna mtu amesimama? *Okay,* ahsante sana. Mheshimiwa Halima halafu Mheshimiwa Mchungaji Msigwa.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi. Nilikuwa nahitaji ufafanuzi kwa sababu miongoni mwa hoja ambazo umezungumza ni kuhusiana na suala zima la *Corona* na kuona ni namna gani kama Bunge tumechukua *initiatives* ambazo tunadhani zinaweza zikatusaidia kuweza kupunguza maambukizi.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nadhani kuna umuhimu wa kwenda mbele zaidi kwa sababu ndiyo Bunge la kwanza tumekaa baada ya janga hili kuikumba dunia. Mabunge yote duniani ambayo janga hili limeyakumba wamelichukulia hili jambo kwa uzito mkubwa na wa kipekee sana.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naomba katika hoja hiyo ya kutafuta ufafanuzi, tunaweza kupata ufafanuzi kutoka kwenye Kiti chako; katika kipindi hiki cha Bunge kitakachokuwa kinaendelea, nilidhani ni busara Serikali kupitia Wizara ya Afya ije Bungeni itoe taarifa ya kina kabisa kuhusu suala la *Corona* Tanzania hali ikoje na *measures* zilizochukuliwa.

Mheshimiwa Spika, unasema *social distancing,* lakini *practicability* ya *social distancing* ni kwa *middle class* na *a privillaged class,* lakini kule uswazi *the so called social distance is not there;* kuanzia kwenye daladala, kwenye mwendokasi ni *total chaos.*

Mheshimiwa Spika, sasa nilidhani kwamba ni muhimu hili suala tulijadili kwa kina ili tuangalie vilevile Serikali ina mpango gani wa dharura wa kibajeti. Wenzetu huko wakisema *total isolation* ama *total lock down* ni kwamba Serikali inafidia wananchi, Serikali inafidia wafanyabiashara, kwa hiyo, kunakuwa kuna *package* mahususi. Unaponiambia Halima nisiendele kwenye kibarua, maana yake najua kama nilikuwa napata kwa mwezi 1,000/= Serikali ina-*provide* hata robo ya ile ili niweze kutulia nyumbani.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili suala ni muhimu. Jana nilipata bahati ya kuwa pamoja na wewe kwenye Kikao cha Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti. Bajeti ya Afya, utekelezaji wake ni *crisis*. Sasa kama leo Serikali imeweza ku--*perform only 15%* ya *total budget* kwenye Wizara nyeti kama ya Afya, hivi *Corona, can we manage* hii *crisis?*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tukija kuzungumza ninadhani tunaweza tukaishauri vizuri Serikali, ili *kits* za kupimia; leo Wabunge ambao tunasema ndio Wawakilishi wa

Wananchi wote inabidi tusambazwe huko, lakini labda tungepimwa ili ijulikane Mheshimiwa Halima kama una *Corona* nipelekwe *caranteen,* ili wabaki watu hapa wafanye kazi. Bila hivyo, leo Wabunge wako kwenye vyumba, lakini kwa nini tusianze na sisi tupimwe wote, tukijijua tuko salama, tukae hapa tu--*debate.*

Mheshimiwa Spika, hili ndiyo Bunge la mwisho kuelekea Uchaguzi Mkuu, kwa hiyo, nilikuwa nakuomba sana sana na ninashukuru kwamba umechukua *measures* kama Spika wetu kuanza kuangalia nini tunafanya sisi kama viongozi tuweze kusalimika. Nadhani kama nchi, kuna hatua kubwa ambazo lazima zichukuliwe, lakini haziwezi kuchukuliwa bila kupata *proper reports,* tuulize maswali, tujibiwe, tushauri, ili tuweze kuokoa wananchi wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama Marekani dunia ya kwanza inatapatapa, kama Italia dunia ya kwanza inatapatapa, kama Spain;

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kutambua kwamba, unajua hili jambo ni kubwa, tuweze kulipatia nafasi tulijadili ili tushauriane, tuweze kuokoa kizazi chetu.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Peter Msigwa, nilikuona.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Siko mbali sana na Mheshimiwa Halima. Ninashukuru kwamba, Serikali imechukua hatua. Kimsingi hii ni vita ambayo lazima kama Taifa tushirikiane kwa pamoja kupambana na tatizo hili. Kwa sehemu ambapo amezungumza Mheshimiwa Halima, tusipokuwa waangalifu inaweza ikaanza kumdondosha mmoja mmoja katikati yetu.

Mheshimiwa Spika, tatizo ninavyoliona, tunaweza tukajitahidi hapa sisi kama Bunge tukawa na hii *social distancing,* lakini ukiangalia kiukweli kwenye mazingira ya huko nyumbani hali bado ni ngumu sana. Kwa hiyo, unaweza ukakuta unatoka hapa, ukirudi nyumbani unaweza ukaleta.

Mheshimiwa Spika, nilichotaka kusema nikiungana na hoja aliyoisema Mheshimiwa Halima, nataka tuichukulie *this is a paramount* kama Taifa na kama Wabunge tujadiliane, kwa sababu, sio suala la ugonjwa tu, lakini kiuchumi tuko *affected big time.* Ni lazima Serikali ije hapa ituambie sisi kama Wawakilishi wa Wananchi ina mipango gani kwa mfano hasa baada ya masuala ya utalii kuporomoka? Watalii hawapo, mapato hayapo; Serikali ije na mpango kwa pamoja tushauriane njia gani tutapita ili tuweze kushikamana kwa pamoja kujikwamua katika tatizo hili. Tukienda kidogo kidogo hivi haiwezi kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, mambo mengi ameyazungumza Mheshimiwa Halima. Nilidhani Serikali ingekuja na mpango tushauriane tuweze kushirikiana kwa pamoja namna gani tunaweza kuchomoka.

Mheshimiwa Spika, ukienda kwenye daladala; kuna *clip* moja jana imepita, wale watu wanang'ang'aniana samaki, mtaponaje? Kwenye *ferry* watu wamejazana hivi, unasemaje mnapoona katika tatizo kama hili kwa ugonjwa wa aina hii?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, haya ni mambo ambayo lazima tujadili kiuwazi kama Wawakilishi wa Wananchi, ili tuweze kutoa mawazo ya pamoja, tuweze kujiokoa katika vita hii.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge. Wote wawili mmeongea *almost* kitu kile kile na msisitizo wenu ni kwamba tujadiliane, tushauriane na ndiyo maana ya neno Bunge na bahati nzuri sisi ndio Wawakilishi

wa Wananchi. Kwa hiyo, Mkutano wetu huu ndio fursa ya kujadiliana na kushauriana. Nami naamini mahali ambapo tuna vita kubwa namna hii tunapaswa kuwa wamoja na kila mmoja lazima atasikiliza kwa umakini mkubwa na kuchukua hatua, lazima kabisa. *(Makofi)*

Kwa hiyo, niwatie moyo Waheshimiwa Wabunge wote, hapa ndiyo mahali pake. Bahati nzuri hiyo kesho tunaanza na hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, ofisi ambayo ndiyo inaratibu mambo yote haya. Kwa sababu, jambo hili la *Corona* ni jambo mtambuka, linahusu Wizara zote na kadhalika na wananchi wote, hapo ndiyo pa kuanzia hiyo kesho.

Pia kupitia Kamati yetu ya Huduma za Jamii na Kamati nyingine zote, kama mna jambo lolote la ushauri mnaweza kulipeleka moja kwa moja, mnaweza kulileta kwa Spika na mnaweza kulifikisha kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Sisi Wabunge tuna nafasi ya kuweza kufanya hivyo na ningependa kutoa wito tufanye hivyo kadiri inavyowezekana.

Natambua mifano mliyosema ya uswazi na kwingine kwamba *social distance* ni ndogo, ni kweli, lakini nisisitize; *social distance* ya masharti ya ki-*corona* ndiyo ndogo, lakini nirudie pale pale niliposema, mwanadamu ni mtu ambaye wakati wote, muda wote ana-*observe social distance.* Maisha ya mwanadamu ni ku-*observe social distance,* yako hivyo. Uwe uko kwenye treni, uwe wapi, kuna umbali fulani ambao unau-*maintain,* yaani mtu aki-*cross* hicho ni kitu cha kwanza ambacho mwanadamu hakubali kabisa. Kusogelewa; unasimama namna hii, mtu mwingine anakuja mgongoni, lazima utageuka tu, nani huyu? Anafanya nini? Kuna nini?

Kwa hiyo, ushauri ni kwamba, tuwaelimishe wananchi wetu hata kama ni mahali gani, wajaribu kuona kwamba hili boti limejaa, basi hebu mimi nisipande kwanza nisubiri boti inayofuata. Bahati nzuri hata kwenye maboti kunakuwa ni mahali pa wazi, mahali ambapo kuna upepo unapita kidogo, na kadhalika, yaani tufuate ushauri wa watu wetu wa kiafya.

Tukumbuke hatuwezi kuchukua *measures* za Wazungu tukazi-*copy* na *ku-paste* hapa kama zilivyo, ni ngumu sana, tutaua watu wetu. Wako watu wanaishi siku kwa siku. Kwa hiyo, lazima tuangalie mazingira yetu ya Kitanzania na tutajaribu kuchukua hatua kufuatana na mazingira yetu. Kama ambavyo sisi Bunge tumeangalia mazingira yetu, tukaona tunawezaje kuendelea kufanya kazi katika mazingira yetu na tukaona tuje na hii *modal* ambayo tunajaribu kui-*practise.*

Kwa hiyo, wenzetu, kila mtu mahali pake ajaribu kufanya hivyo hivyo. Waliko kwenye masoko, yana uongozi wajaribu kuona namna gani nao wanaweza kuchukua hatua fulani fulani, kuweka maji ya kunawa, kuchukua hatua mbalimbali za kuhakikisha kwamba wanapunguza misongamano kwa kadiri inavyowezekana.

Hata wananchi wenyewe tu, ukiona pale pana msongamano, basi upite njia nyingine, ufuate huduma yako kwa namna tofauti na kadhalika, kuliko kujazana pale halafu utegemee Polisi wapige viboko kama inavyotokea kwenye nchi nyingine. Ikilazimika hapo, Serikali itafanya, lakini hatuishauri kwa sasa. Tunajaribu kuelimisha zaidi na kutoa wito na kumwomba Mwenyezi Mungu atuepushie janga hili kubwa ambalo kwa kweli limetingisha hata nchi zenye uchumi mkubwa.

Habari ya kupimwa, ni wazo zuri tulichukue. Tutaongea na wenzetu Serikalini tuone inakuwaje. Maana hata huko kwenye *central laboratory* kutakuwa na *samples* nyingi sasa hivi kuliko wakati mwingine wowote na zitakuwa zikiongezeka kuingia kule. Kwa hiyo, wana kazi kweli hata wataalam wetu kule, kwa hiyo, watatushauri tuone nini cha kufanya. Kama linawezekana, ni jambo jema tu, kwa sababu, bahati nzuri upimaji wake wala hauna ugumu kama upimaji wa magonjwa mengine. Upimaji wa hii zaidi wanatumia *swab;* ka-pamba kale wanaweza kuchukua mdomoni hapa au nini, basi wamemaliza. Anaweka kwenye darubini sijui hadubini, basi unapata majibu baada ya muda ambao unatakiwa.

Kwa hiyo, hili la kupimwa wala halina shida sana.

Kuhusu masuala ya ushauri wa *package* mahususi, bajeti ya Afya na utekelezaji wake, na kadhalika, ndiyo mambo ambayo hata kwenye Kamati ya Bajeti tumesisitiza na ndiyo kipindi chenyewe hiki ambacho Wabunge mna nafasi sasa ya kuweza kuweka *pressure* yenye afya. Naamini kabisa na Serikali nayo itasikiliza.

Waheshimiwa Wabunge kwa kumalizia tukumbuke kwamba, huko nyuma uendeshaji wa Bunge hili la bajeti ulikuwa tofauti na tunavyoendesha kuanzia na Bunge la Mheshimiwa Mama Makinda katikati na Bunge hili. Kule nyuma ilikuwa tukifika Bunge la bajeti kama hivi, Bunge linafunguliwa Jumanne kama leo, Jumatano kesho, Alhamisi Waziri wa Fedha anasoma bajeti ya Serikali. Ndivyo ilivyokuwa. Bajeti ya Serikali ikishasomwa, zinafuata sasa Wizara kwa Wizara, lakini hampunguzi kitu *essentialy* wala hamwezi kuongeza kitu kwa sababu, bajeti inakuwa iko *fixed,* iko pale *rigid.* Unachoweza Mbunge ni kung'ang'ana na shilingi moja tu ya Waziri ambayo haibadilishi chochote katika bajeti ya Wizara.

Tukaenda na mfumo huo tukafika mahali tukasema hapana, mfumo huu sio shirikishi, tukaja na mfumo huu wa sasa. Ndiyo maana tukaunda Kamati inayoitwa Kamati ya Bajeti na Kamati nyingine tukaunda ushirikishi ili kuwe na majadiliano na kuambiana na upande wa Serikali eneo hili tunahisi halijakaa sawa, eneo hili halijakaa sawa, eneo hili halijakaa sawa, ili inapofika tarehe sasa ya Waziri kusoma bajeti ya Serikali, bajeti ile Waziri wa Fedha anayoisoma inakuwa ni bajeti shirikishi kwa sababu, imechukua na baadhi ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge.

Kwa hiyo, tunatoa wito tu kwa pande zote, toa maoni na Serikali kuwa tayari kusikiliza kwa sababu, ndiyo makusudio ya mpango huu wa kwamba kinachosomwa mwisho kiwe ni chetu kisiwe cha upande mmoja au cha watu wachache, hata kidogo. Kwa hiyo, majadiliano ya pande zote mbili ni kitu ambacho kinatiwa moyo sana na tuendelee kukifanyia kazi na ndiyo maana tuliubadili huu mfumo ukaja kwenye

hatua hii tuliyoifikia. Vinginevyo hata kuunda hizi Kamati za Bajeti, na kadhalika, itakuwa ni *non-starter.*

Kwa hiyo, ninatoa wito kwa kusikilizana pande zote mbili na kuzingatia sana ushauri ambao tunapata na Waheshimiwa Wabunge sasa mjipange msome vizuri na uchangiaji wetu wa kwenye bajeti uwe tofauti. Ingawaje kwenye bajeti tunaruhusiwa tu kuchangia chochote, lakini utakuwa umeshapata haya makabrasha, randama na kila kitu. Ni vema zaidi Mbunge ukajielekeza kwenye bajeti kuliko ukisimama una yako tu, inakuwa ni kupoteza muda na fedha za wananchi. Itakuwa ni vizuri zaidi Waheshimiwa mkajiandaa kwa sababu tayari mtakuwa na kila kitu kwenye *tablets* zenu.

Naambiwa Mheshimiwa Mchengerwa alisimama, ni kweli? Haya basi, nikupe nafasi ya mwisho kabisa.

**MHE. MOHAMED O. MCHENGERWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na maelezo mazuri kuhusu namna ambavyo Serikali imejipanga kupambana na *Corona,* yako maafa mengine ambayo Taifa letu linaendelea kukumbwa, ni maafa haya ya mafuriko. Nchi yetu yote imekumbwa na mafuriko na mafuriko haya yamesababisha maumivu makubwa kwa binadamu, wanyama, miundombinu na vitu vingine vingi.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba nchi yetu yote imekumbwa na mafuriko, yako maeneo ambayo mafuriko yamekuwa ni makubwa sana na yamesababisha maumivu makubwa sana kwa wananchi wetu. Eneo hili ni eneo la Rufiji, ambapo wananchi zaidi ya 20,000 mpaka 50,000 wamekuwa *displaced,* hawana pa kuishi, hawana vyakula na wanahangaika sana kuokoa maisha yao.

Mheshimiwa Spika, je, kama Bunge, tunachukua hatua gani ili kuwaangalia hata hawa wananchi wanyonge ambao nao pia wako kwenye maafa ya mafuriko?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchengerwa. Kwanza kupitia kwako Mbunge wa Rufiji na kupitia kwa Mbunge wa Kibiti tunawapeni pole sana; mtufikishie pole hizo

kama Bunge kwa wananchi wetu. Mafuriko yale hayajapata kutokea, ni maafa makubwa sana.

Ujumbe wako ni kwa Serikali, naamini kabisa Serikali imesikia na imekuwa ikiendelea kuchukua hatua na wakati fulani utafika ambapo tutaomba Serikali watu-*update* kidogo ni mambo gani ambayo yanaendelea ili tuweze kujua nafasi ya Watanzania wengine wote kuweza kuona namna gani ya kusaidiana na wenzetu hawa waliopatwa na tatizo kubwa sana la mafuriko.

Kwa hiyo, tunapokea ushauri wako Mheshimiwa Mbunge na Mheshimiwa Jenista ambaye ndio Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, nadhani masuala ya maafa yako chini yake, wakati fulani utakapofika atatu-*update* kama Bunge kuhusiana na nini kinachoendelea, nini kifanyike na ushauri wa Serikali na hatua ambazo zimechukuliwa.

Naomba nishukuru sana na kwa maana hiyo tuweze kumalizia shughuli zetu za leo kwa hatua hiyo.

## MASWALI NA MAJIBU

*(Maswali yafuatayo yaliulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 1

### Kituo cha Afya Bwisya Kupandishwa Hadhi

**MHE. JOSESPH M. MKUNDI** aliuliza:-

Kituo cha Afya Bwisya kimekarabatiwa na kuongezewa miundombinu muhimu kufikia kiwango cha hospitali:

Je, kwa nini Serikali isipandishe hadhi kituo hicho na kuwa Hospitali ili kuimarisha utoaji wa huduma za afya kwa wakazi wa visiwa vya Ukerewe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kuanzia Julai, 2017 hadi Machi, 2020 Serikali imetoa kiasi cha shilingi milioni 800 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe kwa ajili ya ujenzi wa Vituo vya Afya Bwisya na Muriti. Vilevile Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alielekeza baadhi ya kiasi cha fedha za maafa ya ajali ya Kivuko cha Ukerewe kiasi cha shilingi milioni 860 zitumike kupanua na kuboresha miundombinu ya Kituo cha Afya Bwisya. Hivyo kituo hicho kimejengwa na kukarabatiwa kwa jumla ya shilingi bilioni 1.26.

Mheshimiwa Spika, Serikali inakamilisha taratibu za kukipandisha hadhi Kituo cha Afya Bwisya kilichopo kwenye Kisiwa cha Ukara ili kiwe na hadhi ya Hospitali ya Halmashauri.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na miundombinu mizuri iliyopo katika Kituo cha Bwisya, kuna upungufu mkubwa wa watumishi pale kituoni na kuathiri utoaji wa huduma.

Mosi, je, ni lini Serikali itapeleka madaktari na wahudumu wengine wa afya Bwisya?

Pili, Hospitali ya Wilaya ya Ukerewe (Nansio), Vituo vya Afya na Zahanati Jimboni Ukerewe vina upungufu mkubwa wa watumishi (chini ya 50%): Ni lini Serikali itapeleka watumishi wa kutosha na hasa ikizingatiwa ugumu wa jiografia ya visiwa vya Ukerewe?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imepata kibali cha kuajiri madaktari 610 na kuwapanga

kwenye vituo vya kutolea huduma za afya nchini kwa kutoa kipaumbele kwenye maeneo yenye upungufu mkubwa. Hivyo baadhi ya Madaktari hao watapangwa kwenye Vituo vya kutolea huduma za Afya Wilaya ya Ukerewe.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuajiri wataalam wa huduma za Afya kwa awamu kwa kadri ya upatikanaji wa fedha.

Na. 2

**Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo Kushindwa Kutimiza Ahadi Zao**

**MHE. DAVID E. SILINDE** aliuliza:-

Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo wamekuwa wakishindwa kuleta misaada na ahadi zao kwenye utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo kwa wakati na nyakati nyingine kushindwa kuleta kabisa katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha mfululizo iliyopita ya 2016/2017, 2017/2018 na 2018/2019:-

Je, Serikali inatueleza ni kitu gani kinasababisha hali hii?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa ikishirikiana na nchi Wahisani pamoja na Washirika wa Maendeleo katika kutekeleza Bajeti yake kwa kupokea fedha za Bajeti ya Maendeleo kupitia Misaada na Mikopo nafuu kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo kuanzia 2016/2017 hadi 2018/2019 Washirika wa

Maendeleo wamekuwa wakitimiza ahadi zao kwa wastani wa zaidi ya asilimia 77 kwa mtiririko ufuataao:-

Mheshimiwa Spika, mwaka 2016/2017 kiasi kilichopokelewa kutoka kwa Washiriki wa Maendeleo kilikuwa ni shilingi bilioni 2,474 sawa na asilimia 69 ya lengo la kipindi hicho la kupokea shilingi bilioni 3,601; mwaka 2017/2018 kiasi kilichopokelewa kilikuwa ni shilingi bilioni 3,351 sawa na asilimia 84 ya lengo la kipindi hicho la kupokea shilingi bilioni 3,971; na mwaka 2018/2019 kiasi kilichopokelewa kilikuwa ni shilingi bilioni 2,082 sawa na asilimia 78 ya lengo la kipindi hicho la kupokea shilingi bilioni 2,676.

Aidha, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Februari, 2020 fedha za misaada na mikopo nafuu zilizopokelewa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimefikia jumla ya shilingi bilioni 1,631.19 sawa na asilimia 90 ya lengo la kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizi, siyo sahihi hata kidogo kusema kwamba kuna nyakati nyingine Washirika wa Maendeleo wamekuwa hawatimizi ahadi zao kabisa.

**MHESHIMIWA DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya ngongeza.

(a) Ni kwa nini sasa fedha za Wahisani zinachelewa kufika kwa wakati na nyingi zinakuja wakati tunamaliza mwaka wa fedha?

(b) Naomba sasa Serikali itoe orodha ya nchi wahisani ikionesha mwenendo wa walichochangia katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha iliyopita?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo hutoa fedha kulingana na makubaliano ya kimkataba yaliyopo kati ya Serikali na washirika hao. Kwa kutambua hilo, baadhi ya Washirika wa Maendeleo hutoa fedha mwishoni mwa mwaka wa fedha wa Serikali kutokana na kupishana kwa kalenda kati ya mwaka wa fedha wa Serikali na kalenda za mwaka wa fedha wa Washirika wa Maendeleo, jambo ambalo Serikali hulizingatia katika mipango yake.

Hivyo basi, siyo kweli kwamba fedha za wahisani zinachelewa kufika kwa wakati. Fedha hizo hutolewa kwa mujibu wa mikataba hiyo ambayo inaainisha muda ambao Washirika wa Maendeleo wanatakiwa kutoa fedha hizo ili kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa na Serikali.

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha miaka mitatu iliyopita (2016/2017 – 2018/2019), Serikali imekuwa ikipokea fedha za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kutoka kwa nchi wahisani kwa kiwango cha kuridhisha kutoka kwa nchi wahisani pamoja na Washirika wa Maendeleo wakiwemo Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Umoja wa Ulaya, Japan, Korea, India, Finland, Ufaransa, Ujeruman, *Global Fund, IFAD,* Norway, Umoja wa Mataifa *(UN)* pamoja na Sweden.

Aidha, orodha ya nchi wahisani pamoja na Washirika wa Maendeleo ikionesha mwenendo na kiasi walichochangia kwa kipindi hicho tutaiwasilisha kwa Mheshimiwa Mbunge baada ya kufanya uchambuzi wa kina kama alivyoomba.

Na. 3

**Kurasimisha Shughuli za Ufugaji Nchini**

**MHE. DKT. IMMACULATE S. SEMESI** aliuliza:-

Tanzania ni kati ya nchi zenye mifugo mingi barani Afrika na sekta hii inaweza kuikwamua nchi kiuchumi:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kurasimisha au kuboresha shughuli za ufugaji nchini ili uwe wa kisasa na wenye tija zaidi badala ya ufugaji wa kuhama hama?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** atajibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, asilimia 97 ya mifugo hufugwa kwa mfumo wa asili ambapo kaya milioni 4.6 sawa na asilimia 50 ya kaya zote vijijini hufuga mifugo. Wizara ya Mifugo na Uvuvi inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza mchango wa Sekta ya Mifugo kwenye Maendeleo ya Jamii na Pato la Taifa kwa kuleta tija katika uzalishaji, usindikaji na hatimaye soko la mifugo na mazao yake.

Mheshimiwa Spika, mikakati inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na:-

(i) Mkakati wa kuzalisha wingi ng'ombe bora wa maziwa na nyama kwa njia ya uhimilishaji.

(ii) Mkakati wa upatikanaji wa uhakika wa malisho na maji kwa mifugo.

(iii) Mkakati wa kudhibiti na kuondoa migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

(iv) Mkakati wa udhibiti wa magonjwa ya mifugo kwa njia ya kinga (uogeshaji na chanjo) na tiba.

Mheshimiwa Spika, aidha, Wizara imeendelea kutoa mafunzo juu ya teknolojia sahihi za uzalishaji kwa wafugaji na Maafisa Ugani katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Na. 4

**Hitaji la Wataalam wa Mifugo na Maabara za Mifugo Nchini**

**MHE. JUSTIN J. MONKO** aliuliza:-

Mifugo ya Wafugaji wakubwa hapa nchini imekosa ubora wa mazao yake kutokana na maradhi yanayochangiwa na kukosekana kwa wataalam waliobobea katika fani na kukosa Maabara za Mifugo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza wataalam ama vitendea kazi kama njia mbadala ya kuwasaidia wataalam wachache waliopo kutoa huduma bora kwa wafugaji?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga maabara za mifugo katika maeneo ya wafugaji ili wananchi waache kutibu mifugo yao kwa kubahatisha?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Justin J. Monko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inafanya juhudi za kuongeza idadi ya Maafisa Ugani wa mifugo kwa kuwezesha Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo *(LITA)* kuongeza udahili wa wanafunzi wa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika fani za uzalishaji, afya ya mifugo, nyanda za malisho na maabara kutoka wanafunzi 2,536 mwaka 2018/ 2019 hadi wanafunzi 3,634 mwaka 2019/2020; sawa na ongezeko la wanafunzi 1,098 ambalo ni asilimia 43.3.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na mpango wa ujenzi wa maabara za mifugo kwenye kila mkoa. Mpaka sasa kuna maabara za mifugo za Serikali kumi na moja kwenye kila Kanda. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara inategemea kujenga Kliniki za mifugo zenye maabara katika

Halmashauri mbili za Chato na Meatu. Aidha, katika mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara imepanga kujenga Kliniki nyingine kumi kwenye Halmashauri mbalimbali nchini ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Sindiga Vijijini.

Mheshimiwa Spika, Wizara pia imeshavielekeza vituo binafsi 1,709 vya kutolea huduma ya afya ya mifugo *(Private Veterinary Centers)* vilivyopo kwenye Halmashauri zote 185 kuhakikisha vinakuwa na maabara ndogo kwa ajili ya kutoa huduma ya uchunguzi wa awali wa magonjwa ya mifugo.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi ambazo Mheshimiwa Waziri amezieleza, kukosekana kwa miundombinu ya uogeshaji wa mifugo kumechangia katika kudumaza afya za mifugo na uboreshaji wa majosho nchini umekuwa kwa kasi ndogo sana:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa muda mfupi wa kuboresha majosho nchini katika maeneo ya wafugaji?

(b) Wizara ina mkakati gani wa kuhakikisha chanjo hizi muhimu zinapatikana kwa urahisi wakati wote?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020 jumla ya majosho 292 yamekarabatiwa nchini. Kati ya hayo, 161 yamekarabatiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi na 131 yamekarabatiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Majosho hayo yapo katika mikoa ya Singida, Iringa, Kagera, Katavi, Kigoma, Mara, Mwanza, Rukwa, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu na Tabora.

Aidha, Wizara imetoa maelekezo kwa Halmashauri zote nchini kukarabati miundombinu ya mifugo yakiwemo majosho kwa kutumia fedha inayotokana na mapato ya ndani kutoka katika Sekta ya Mifugo.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara imetenga kiasi cha shilingi 100,000,000/= kwa ajili ya kukarabati majosho 125 katika Halmashauri za Wilaya 25 ikiwemo Singida.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeendelea kuimarisha uzalishaji wa chanjo ndani ya nchi ambapo uzalishaji wa aina za chanjo katika Kiwanda cha Kuzalisha Chanjo za Mifugo *(TVI)* cha Kibaha umeongezeka kutoka chanjo aina nne mwaka 2018/2019 kufikia chanjo aina sita kwa mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, aidha, jumla ya dozi 49,008,325 za chanjo zikiwemo dozi 47,347,700 za chanjo ya matone dhidi ya Ugonjwa wa Mdondo *(TEMEVAC - $I_2$)*, dozi 626,000 za Ugonjwa wa Kimeta, dozi 113,000 za Ugonjwa wa Chambavu, dozi 756,600 za Ugonjwa wa Mapafu ya Ng'ombe, dozi 19,275 za Ugonjwa wa Kutupa Mimba na dozi 145,750 za chanjo zenye muunganiko wa Kimeta na Chambavu *(combination of Blackquarter vaccine and Anthrax vaccine - TECOBLAX)* zimezalishwa na kusambazwa kwa wadau nchini.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeandaa utaratibu wa manunuzi ya chanjo kwa pamoja *(Bulk Procurement)* ambapo chanjo zote ambazo hazizalishwi hapa nchini zitaingizwa nchini ikiwemo chanjo za Magonjwa ya Mapele, Ngozi, Miguu na Midomo kwa pamoja na zitakuwa na bei elekezi na zitasimamiwa na Serikali ili kupunguza gharama ya chanjo kwa wafugaji.

Mheshimiwa Spika, aidha, kwa Mkoa wa Singida chanjo zinapatikana katika Kituo cha *TVLA* Kanda ya Kati kilichopo Dodoma.

Na. 5

**Ujenzi wa Uwanja wa Michezo – Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Serikali ilipata ufadhili wa kujengewa uwanja wa michezo Mkoani Dodoma kutoka Serikali ya Morocco.

Je, ni lini uwanja huu wa Michezo utaanza kujengwa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mfalme Mohamed VI alipofanya ziara yake katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Oktoba, 2016 alitoa ahadi ya kufadhili miradi mbalimbali nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa msikiti mkubwa na ujenzi wa uwanja wa kisasa wa michezo nchini. Baadhi ya ahadi kama ujenzi wa msikiti zimeshakamilika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ujenzi wa uwanja wa michezo wa kisasa, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliamua uwanja huo ujengwe katika Jiji la Dodoma eneo la Nane Nane. Maandalizi yote ya msingi ikiwa ni pamoja na kutenga eneo lenye jumla ya ekari 328.6, kupima eneo lote la mradi, kufanya tathmini ya mazingira na kijamii *(Environmental and Social Impact Assessment)*, *topographical survey, geotechnical survey* na kuandaa mchoro wa awali wa uwanja tarajiwa yamefanywa.

Mheshimiwa Spika, kimsingi maandalizi ya awali ambayo yalipaswa kufanywa na Serikali ya Tanzania yamekamilika kwa kiasi kilichokusudiwa. Aidha, mawasiliano baina ya Serikali mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ile ya Morocco kuhusu kukamilisha mradi huu yanaendelea.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu Mazuri ya Serikali naomba kuuliza maswali mawili ya Nyongeza. Kwa kuwa Mfalme wa Morocco alikubali kujenga Uwanja wa Michezo wa Kimataifa hapa Dodoma:

Je, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iko tayari kuwasiliana na Serikali ya Morocco ili ujenzi uanze mapema iwezekavyo?

Kwa kuwa Dodoma ndiyo Makao Makuu: Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga viwanja vingine vya michezo ili ikiwezekana Tanzania ije ipate nafasi ya kuwa Mwenyekiti wa Michezo ya Kimataifa.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi, mawasiliano baina ya Serikali mbili za Tanzania na ile ya Morocco yanaendelea na ni tumaini letu kwamba muafaka utafikiwa mapema iwezekanavyo kuhusu mradi huu wa ujenzi wa uwanja wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, pili, kwa kuwa bado mpango wa kujenga uwanja mpya wa Dodoma unaendelea, Mheshimiwa Mbunge avute subira kwa sasa Serikali ikamilishe kwanza mradi huo na kisha Serikali itaweza kufikiria kujenga viwanja vingine zaidi na siyo lazima iwe Dodoma pekee, bali hata miji mingine inayozunguka Makao Makuu ya nchi itafikiriwa.

Na. 6

**Ukamilishwaji wa Jengo la Kituo Kipya cha Polisi Dunga**

**MHE. ASHA MSHIMBA JECHA** aliuliza:-

Azma ya Serikali ya kuwafikishia wananchi huduma popote walipo ni njema. Aidha, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa Kituo kipya cha Polisi Dunga baada ya jengo la awali kuwa bovu na kuvunjwa.

(a) Je, ni lini jengo hilo jipya litakamilishwa kwa kufanyiwa matengenezo yaliyobaki?

(b) Je, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi iko tayari kukipatia Kituo cha Polisi Dunga gari la huduma?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ujenzi wa Kituo cha Polisi Dunga Daraja C ulianza mwezi Julai, 2018 na ulisimama mwezi Novemba, 2018 ukiwa umefikia hatua ya umaliziaji *(finishing)* ambayo tathmini yake inakadiriwa kufikia shilingi 49,862,220.

Mheshimiwa Spika, Jeshi la Polisi linategemea kupata fedha hizo kutoka katika Mfuko wa tuzo na tozo na zitatumiwa katika mfumo wa nguvu kazi *(Force Account)*.

(b) Mheshimiwa Spika, Kituo cha Polisi Dunga kipo katika Wilaya ya kati Mkoa wa Kusini Unguja. Mkoa mzima una jumla ya magari ya Polisi 17. Wilaya ya kati peke yake ina magari mawili mazima. Jeshi la Polisi limekuwa likigawa magari kwa awamu kwa kadiri yanavyopatikana. Kituo cha Polisi Dunga ni miongoni mwa vituo vitakavyopatiwa magari pindi yatakapopatikana.

Na. 7

**Hitaji la Umeme Vijiji vya Mpepai na Lipilipili**

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Vijiji vya Mpepai na Lipilipili?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wakala wa Nishati Vijijini *(REA)* inatekeleza mradi wa kusambaza umeme vijijini katika vijiji vyote vya Tanzania Bara. Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Juni, 2021. Mradi wa

*REA III* unaoendelea utapeleka umeme katika vijiji 50 vya Wilaya ya Mbinga kupitia Mkandarasi *Namis Corporate Ltd* anayetekeleza kazi hiyo katika Mkoa wa Ruvuma.

Mheshimiwa Spika, Vijiji vya Mpepai na Lipilipili pamoja na vijiji vingine vilivyobaki katika Wilaya ya Mbinga vitapatiwa umeme kupitia Mradi unaoendelea. Kazi ya kupeleka umeme katika vijiji vya Mpepai na Lipilipili inahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 yenye urefu wa kilomita 18, ujenzi wa njia ya msongo wa kilovoti 0.4 yenye urefu wa kilomita 22, ufungaji wa transfoma nane za KVA 50, 100 na 200, pamoja na kuwaunganishia huduma ya umeme wateja wa awali 313. Gharama ya mradi ni shilingi milioni 977.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa chanzo cha umeme cha maji cha Tulila kipo katika Kata ya Mpepai na miundombinu yake inapitia katika Kitongoji cha elfu mbili na vijiji vya Kata za Mapendano kuelekea Songea, Serikali haioni umuhimu wa kuvipatia Vijiji vya Kata za Mpepai na Kihungu umeme kwanza kabla ya vijiji vingine hasa ukizingatia vijiji hivyo hulinda na kuitunza miundombinu hiyo na hivyo kuwafanya wananchi wa Mpepai kupata hisia za kuwa wametengwa na kubaguliwa kwenye huduma hiyo ya umeme?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli miundombinu ya umeme kutoka katika chanzo cha maji cha Tulila inapita katika Kata za Mpepai na Kihungu. Katika Kata ya Kihungu kuna Vijiji vya Pachasita na Kihungu ambavyo tayari vimeunganishwa na huduma ya umeme. Kijiji kimoja cha Lipembe kitapatiwa umeme kupitia mradi wa *REA III* unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika jibu la msingi kuwa kupitia utekelezaji wa mradi wa *REA III*, Mzunguko wa pili, vijiji vyote vya Kata ya Mpepai ambavyo ni Lipilipili, Luhangai, Mtua, Mpepai na Ruvuma chini vitapatiwa umeme.

Na. 8

**Kesi Kuchukua Muda Mrefu Kusikilizwa**

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF** aliuliza:-

Mfumo wa Mahakama umejiwekea utaratibu wa kuanza na kuamaliza mashauri ambapo kwa Mahakama ya Rufaa na Mahakama Kuu ni miaka miwili, Mahakama za Mahakimu Wakazi ni mwaka mmoja na Mahakama za Mwanzo ni miezi sita. Utaratibu huu ni mzuri ambao unaendana na msemo usemao: "Haki iliyocheleweshwa ni sawa haki iliyonyimwa."

Je, ni kwa nini utaratibu huu haufuatwi na badala yake kesi nyingi zinachukua muda mrefu?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Suleiman Ally Yussuf, Mbunge wa Magogoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli Mahakama ya Tanzania imejiwekea utaratibu wa kuhakikisha mashauri yote ambayo yanafunguliwa Mahakamani yanakuwa na muda maalum wa kukamilika katika ngazi husika za Mahakama kama yalivyo maelezo kwenye Swali la Msingi la Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu kwa kiasi kikubwa umesaidia kupunguza changamoto ya mlundikano na mashauri kuchukua muda mrefu kusikilizwa. Pamoja na mfumo huu mzuri, bado kwa baadhi ya Mahakama utaratibu huu umekuwa haufuatwi kutokana na sababu mbalimbali kama idadi ndogo ya Majaji na Mahakimu ikilinganishwa na mashauri yanayofunguliwa Mahakamani, upepelezi kwa baadhi ya mashauri ya jinai kuchukua muda mrefu, maahirisho ya mara kwa mara kutoka kwa Wadaawa wenyewe na sababu nyingine nyingi ambazo zinawagusa

wadau wakubwa wa Mahakama katika uendeshaji wa mashauri.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa, wakati wa maadhimisho ya kilele cha Wiki ya Sheria nchini Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alikemea ucheleweshwaji wa upelelezi katika mashauri mbalimbali na kutaka taasisi zinazohusika kufanya kazi hiyo kwa haraka ili haki za watuhumiwa zipatikane kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Jaji Kiongozi aliwataka Mahakimu wa Mahakama za Wilaya na Mahakama za Hakimu Mkazi nchini kutopokea kesi za jinai ambazo upelelezi au ushahidi wake haujakamilika (Tangazo la Serikali Na. 296 la mwaka 2012). Utekelezwaji wa mwongozo huu utasaidia sana usikilizwaji wa mashauri haraka na hivyo haki kupatikana kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, vilevile ninamshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. Magufuli katika Awamu ya Tano kwa kuteua idadi kubwa ya Majaji wa Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufani.

Mheshimiwa Spika, napenda kulithibitishia Bunge lako kuwa, Serikali kwa kushirikiana na Mahakama, tutaendelea kuhakikisha changamoto hizi zinapungua kwa kiasi kikubwa ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu katika Mahakama zetu.

**MHE. DKT. SULEIMAN ALLY YUSSUF:** Mheshimiwa Spika, moja ya kesi ambayo inavuta hisia ya watu wengi ni kesi ya Mashehe wa Uamsho kutoka Zanzibar ambayo ilianza awamu iliyopita na kurithiwa na awamu hii. Sasa ni zaidi ya miaka saba na hata kuanza bado:-

(a) Je, ni sababu gani iliyosababisha ucheleweshaji huu mkubwa wa uoaji haki?

(b) Je, ni muda gani kesi iliyokosa ushahidi inatakiwa kufutwa?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kesi anayoiuliza Mheshimiwa Mbunge bado ipo Mahakamani na hivyo kwa mujibu wa Kanuni za kudumu za Bunge, suala lolote ambalo lipo Mahakamani haliwezi kujadiliwa Bungeni. Ni vyema tukasubiri vyombo husika vikafanya kazi yake na kutoa maamuzi.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, zipo sababu zinazoweza kusababisha ucheleweshaji wa kukamilika upelelezi wa kesi ya jinai, nazo zinaweza kutokana na sababu zifuatazo:-

(i) Asili na namna kosa lilivyotendeka na wahusika wanaotuhumiwa kutenda kosa hilo iwapo wametenda kosa hilo wakiwa maeneo mbalimbali kwa maana ya kuwa hawakai eneo moja na wana mtandao mkubwa ndani na nje ya nchi.

(ii) Aina ya kosa husika, mathalani kesi yenye viashiria vya ugaidi, utakatishaji fedha, uhujumu uchumi, rushwa na kadhalika. Watu wanaofanya makosa ya aina hii wana mtandao mkubwa ndani na nje ya nchi.

(iii) Upelelezi kuhitaji upatikanaji wa taarifa, nyaraka na mashahidi nje na ndani ya nchi. Katika mazingira hayo upelelezi wake huchukua muda mrefu kukusanya ushahidi huo.

(iv) Mheshimiwa Spika, kesi ambayo haina ushahidi haiwezi kufikishwa Mahakamani. Hata hivyo, kutokana na uzito wa kosa la kesi iliyo katika hatua za upelelezi, kesi hiyo inaweza kukaa muda mrefu katika hatua hiyo kabla ya kuamua vinginevyo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo changamoto za ukusanyaji wa ushahidi ndani na nje ya nchi wa kesi hii, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa sasa hivi taratibu za upelelezi wa kesi hii zinahitimishwa na hivi karibuni hatua za kusikilizwa kwa kesi hii zitaanza.

Na. 9

## Tatizo la Maji Mkoa wa Mtwara

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Tatizo la maji Mkoani Mtwara limeendelea kuwa kero kubwa kwa wananchi wa Mkoa huo:-

(a) Je, mradi wa kutoa maji mto Ruvuma hadi Mtwara Manispaa umefikia hatua gani?

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za ukarabati wa Mradi wa Maji wa Mbuo Nkunwa?

(c) Je, ni nini hatma ya Mradi wa Maji Makonde?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Jimbo la Mtwara Vijijini, lenye Sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali imekamilisha upembuzi yakinifu wa mradi wa kutoa maji katika chanzo cha maji cha Mto Ruvuma kwa ajili ya wakazi wa Mkoa wa Mtwara. Kwa sasa Serikali inatafuta fedha kwa ajili ya kuajiri mtaalam atakayefanya usanifu wa kina na kuandaa makabrasha kwa ajili ya kuanza utekelezaji katika mwaka wa fedha 2020/2021. Mradi huu ni mkubwa, ukitekelezwa utakuwa mkombozi mkubwa kwa wananchi wa Mkoa wa Mtwara.

(b) Mheshimiwa Spika, ukarabati wa mradi wa maji Mbuo – Nkunwa unaendelea kufanyika na Mkandarasi anaendelea na kazi. Mpaka sasa bomba la njia kuu lenye urefu wa kilomita 3.6 limelazwa na wananchi wanaendelea kupata huduma ya maji.

Pia mkandarasi amechimba kisima kingine kipya ili kuongeza kiasi cha maji. Kazi ya kufunga miundombinu ya bomba la mtandao wa maji inaendelea. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Aprili, 2020. Usimamizi wa mradi huu unafanywa na wataalam wa ndani *(force account)* wa Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mtwara *(MTUWASA)*.

(c) Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mradi wa Makonde, Serikali imepanga kufanya ukarabati kwa awamu. Awamu ya kwanza ya ukarabati inaendelea ambapo tayari njia ya bomba kuu yenye urefu wa kilomita 17 kutoka chanzo cha maji Mitema hadi Mjini Newala imekamilika.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ufungaji wa pampu inaendelea ili majaribio ya mradi yafanyike kwa ajili ya Mji wa Newala. Aidha, katika awamu hii upo mpango wa kuongeza njia nyingine kubwa kutokea Mitema hadi eneo la Nambunga ambapo tenki lenye uwezo wa lita milioni tano litajengwa na maji yatasambazwa katika Mji wa Newala na vijiji jirani. Awamu ya pili itahusisha ukarabati wa mtandao wa mabomba katika eneo la Tandahimba ili kutoa huduma ya maji ya uhakika.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba tusimame ili tuahirishe shughuli zetu za Bunge hadi kesho saa 8.00 juu ya alama katika ukumbi huu huu kwa wale ambao watakuwa wamepewa taarifa kwamba wanatakiwa wawemo kwenye ukumbi huu. Ahsanteni sana.

*(Saa 3.45 Asubuhi Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatano Tarehe 1 Aprili, 2020 Saa 8.00 Mchana)*